# MAKARIBISHO

**KARIBU SANA**

**TAG KINONDONI REVIVAL CHURCH**

**Kwako ndugu, mgeni wetu na rafiki yetu uliyetutembelea ili kuabudu pamoja nasi, tunapenda kukuhakikishia kuwa tunajisikia furaha kubwa na kupendelewa na Mungu wetu kuwa pamoja nawe. Kwa hiyo unakaribishwa sana na tafadhali jisikie vizuri kuabudu pamoja nasi.**

**WACHUNGAJI WA KANISA:**

**Askofu Dkt. Rogathe Z. Swai-Mch Kiongozi**

**Mch. Msaidizi - Bryson Kitoi 0755 641497**

**Mch. Msaidizi - Joseph Enos 0652 889852**

**Mch. Msaidizi - Witness Swai 0629 534530**

**Mch. Msaidizi– Yotham Mackenzie 0754266214**

**Mch. Msaidizi– Dickson Mkoka-0718 694495**

**Mch. Msaidizi– Greyson Nyantamba0745238790**

**Anuani yetu: TAG Kinondoni Revival Church**
**S.L.P 1338, Dar es Salaam.**

**Barua pepe : info@krc.or.tz**
**Tovuti : www.krc.or.tz**

**Tafadhali jisikie huru kuwasiliana nasi, tuko tayari kuwasiliana nawe na kukuhudumia.**

**KWAYA ZETU:**

**Kuna kwaya nzuri sana zilizojaa upako mwingi wa Roho Mtakatifu ambazo ni Victory Singers, Kinondoni Revival Choir na Kinondoni Sayuni. Karibu ushuhudie mwenyewe uimbaji uliojaa nguvu za Mungu na utabarikiwa sana.**

0

# MATANGAZO

**VIONGOZI WA ZAMU**

**15 –21 JUNI 2026**

**MCHUNGAJI**

REV. JOSEPH ENOS 0652 889 852

**MZEE WA KANISA:**

**MR. MATHIAS MSANGI**

**WAZEE NA MAKATIBU WAO WATAKAOKUWA WA ZAMU, KUABUDU IBADA ZOTE MBILI SIKU YA JUMAPILI IJAYO TAREHE 21/06/2026:**

**DR. YOTHAM MACKENZIE**

**DR. DICKSON MKOKA**

**MR. JOSEPH MAMUYA**

**MASHEMASI WA ZAMU:**

**MR. LADISLAUS MELKIZEDECK**
**MRS. MAGRETH KATUMBA**
**MRS. MARY C. ZONGELA**
**MRS. MARIAM KASEKA**

**MATANGAZO**

Wazee wote wenye mitaa mnahimziwa kutembelea vituo vyenu vya HBCF ili kujua maendeleo ya vituo hivyo na kuviimarisha, wakisaidiana na makatibu pamoja na mashemasi.

Kutakuwa na Ibada ya shukrani ya nusu mwaka pamoja na Ushirika wa meza ya Bwana tarehe 28.06.2026. Washirika wote tujiandae na ibada hiyo yenye baraka.

Sambamba na hilo pia siku hiyo ya tarehe 28.06.2026 kutakuwa na chakula cha pamoja, hivyo Ibada itakuwa moja na itaanza saa mbili asubuhi.. Kwaya zote zijiandae kuhudumu zikiwemo WWK, CMF na Watoto

Mchungaji kiongozi anakumbusha tena kuwa vijana ambao wako kwenye mahusiano ya uchumba wasikae zaidi ya miezi mitatu bila kuonana na Mch. Dickson Mkoka pia wajitambulishe kwenye kamati ya kushauri chumba na kuhudhuria kwenye vikao vya chumba.

# MATANGAZO

**MICHANGO YA FEDHA ZA UJENZI**

**1.Kwa neema ya Mungu ujenzi wa kanisa letu unaendelea, hivyo unatiwa moyo wewe uliye ahidi mchango wa ujenzi kwa awamu hii ya sita B kutoa au kupunguza ahadi yako ili kazi ya ujenzi iendele. Kumjengea Mungu nyumba ya ibada ni baraka kwako na kwa vizazi vyako.**

**2.**Unaweza kutuma mchango wako kwenda namba:
**015 0020374000 CRDB BANK.**
**Jina: KINONDONI REVIVAL CHURCH**

**PAA LA KANISA, MUUJIZA WANGU**

**ZAMU ZA MAOMBI YA WATENDAJI**

Watendaji wote wa Kundi BETHELEHEMU mtakuwa zamu ya mfungo na maombi siku ya Jumamosi ijayo ya tarehe 20.06.2026. Watendaji wote waliopo maeneo ya Mr. Remigius Ngaiza, Mrs. Rhoda Bundara, Mch. Greyson Nyantamba na Mch. Dickson Mkoka.

**TANGAZO IDARA YA WATOTO**

Tarehe 12.06.2026 : Mkesha wa kusifu na kuabudu, maombi na kuonyesha vipaji vya watoto na maombi ya ujazo wa Roho Mtakatifu. Mzazi njoo tuwaombee watoto wetu chai na maandazi vitakuwepo

Tarehe 15– 21 Juni 2026 wiki ya Idara ya watoto na wanafunzi, kutakuwa na makambi hapa kanisani kuanzia saa 8 mchana hadi saa 12 jioni

Ibada ya Jumatano, Alhamisi na Ijumaa (HBCF) zitaongozwa na Idara ya watoto.Njoo na familia yako yote upokee kutoka kwa Bwana.

Tarehe 20/6/2026 siku ya kuhitimu kambi watoto wote watakuja kanisani kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja jioni, chakula cha mchana kitakuwepo.

Tarehe 21.06.2026 ni kilele cha sikukuu ya watoto, sare ziko tayari (Tshirt) bei ni Tzs 10,000.

## RATIBA YA WIKI

**Jumatatu: 10:30—12:30 Jioni**

- Idara ya Wanawake Watumishi wa Kristo
- Ushirika wa Wanaume Wakristo

**Jumanne:**

- 03:30—08:30 Usiku - (Mkesha)

**Jumatano : 10:30—12:30 Jioni**

- *Kusifu na Kuabudu,*
- Kujifunza Biblia, Maombezi,
- Uponyaji, Ukombozi wa kila aina.

**Alhamisi : 10:30-12:30 Jioni**

Ibada ya vijana

**Ijumaa :**

- Saa 01:00 usiku —04:00 usiku - Maombi ya awamu ya kwanza.
- Saa 04:00 usiku — 10:00 Alfajiri - Maombi ya awamu ya pili (Mkesha)

**Jumamosi:**

- Saa 8:00—10:00 Jioni - Maombi ya watendaji
- Saa 10:00—12:00 Jioni - Mafundisho ya Neno la Mungu (Darasa la wanafunzi makini)

**Jumatatu hadi Ijumaa:**

- Saa 12:00—saa 1:00 Asubuhi

Maombi ya Asubuhi (Morning Glory)

**Jumapili:**

- 12:00—12:50 Asubuhi - Maombi
- 01:00—04:00 Asubuhi - Ibada ya Kwanza
- 04:00—07:30 Mchana - Ibada ya Pili

TAFADHALI KARIBU TENA KUABUDU

PAMOJA NASI

## TAFAKARI YA WIKI HII

**15—21 JUNI 2026**

### WATOTO WAMECHAGULIWA NA BWANA

**Yer 1:7.**

**Lakini BWANA akaniambia, Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru.**

**Waamuzi 13:5**

**5 Kwani tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume; na wembe usipite juu ya kichwa chake; maana mtoto huyo atakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni; naye ataanza kuwaokoa Israeli na mikono ya Wafilisti.**

**1Sam 1:24**

**24 Naye alipokuwa amekwisha kumwachisha maziwa, akamchukua pamoja naye, na ng'ombe watatu, na efa moja ya unga, na chupa ya divai, akamleta nyumbani kwa BWANA, huko Shilo; na yule mtoto alikuwa mtoto mdogo.**

**1Sam 2:11**

**11 Kisha Elkana akaenda Rama nyumbani kwake. Na yule mtoto akamtumikia BWANA mbele yake Eli, kuhani.**

**Mithali 22:15**

**Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto;Lakini fimbo ya adhabu itaufukuzia mbali.**

**Watoto wetu ni watumishi wa Mungu, hivyo Mzazi unawajibika kuwalea sawasawa na Neno la Mungu**

# KINONDONI REVIVAL CHURCH

## UTAKATIFU NDIYO ASILI YETU



**'MUNGU WA MBINGUNI AKUBARIKI UNAPOHUSIKA KIKAMILIFU KATIKA KUFANIKISHA MAONO HAYA'**

**Tunakukaribisha**

Kwa pendo la Calvary
Kumwabudu Mungu Pamoja nasi.

## MATANGAZO YA KANISA

**15—21 JUNI 2026**